

## **Kitabu cha kwanza cha Wafalme**

### **MAZINGIRA YA VITABU VYA WAFALME**

Vitabu viwili vya Wafalme hapo mwanzo vilikuwa kitabu kimoja, navyo vinaendelea na historia ya Israeli tangu mwisho wa vitabu vya Samweli. Muda wote unaoelezwa katika vitabu hivi ni kama miaka 400 hivi, kuanzia miaka ya mwisho ya utawala wa Daudi mpaka watu walipopelekwa katika kifungo cha Babeli. Vinaeleza mgawanyiko wa ufalme katika sehemu mbili, historia yake na jinsi falme hizo mbili zilivyorudi nyuma na kwenda mbali na mapenzi ya Mungu.

### **Alama kuu za vitabu hivyo**

Kama ilivyokuwa katika vitabu vya Yoshua, Waamuzi na Samweli, vitabu viwili vya Wafalme viliandikwa kama historia ya unabii. Maana yake ni kwamba, madhumuni ya mwandishi siyo kusimulia matukio ya historia tu, bali alitaka kuonyesha maana ya matukio hayo katika makusudi ya Mungu. (Kwa maelezo zaidi kuhusu alama ya maandiko ya historia ya unabii, tazama maelezo katika mwanzo wa kitabu cha Yoshua.)

Kwa sababu ya makusudi hayo ya kuonyesha maana ya historia ya Israeli, mwandishi hakisimulia matukio yote ya wakati fulani wala hakuorodhesha mambo yote kwa mfululizo maalumu wa wakati. Yeye alichagua na kupanga habari zake kadiri ya maana yake ya dini kuliko ya kisiasa. Inawezekana kwamba mfalme aliyekuwa na mambo mengi makubwa ya siasa ametajwa kwa maneno machache tu (k.mf.Omri; 1 Fa 16:21-28), ambapo mambo yasiyokuwa ya maana kubwa ya siasa aliyaeleza kwa kirefu (k.mf.huduma za Eliya na Elisha). Alitaja mambo ya nchi za jirani tu kama yalikuwa na maana kwa makusudi ya Mungu kwa ajili ya Israeli.

Mwandishi wa vitabu vya Wafalme hakutajwa kwa jina. Inawezekana kwamba alikuwa nabii mmojawapo, naye labda alipata nafasi ya kusoma masimulizi rasmi ya historia ya kifalme pamoja na masimulizi ya manabii kwa kuandaa maandiko yake (1 Fa 11:41; 15:7, 23, 31; taz. 2 Nya 9:29; 33:19). Sehemu kubwa za vitabu vya manabii Isaya na Yereemia pia zinaonekana katika vitabu vya Wafalme (Isa 36:1-39:8; Yer 39:1-10; 52:1-34). Inawezekana kwamba kazi ile yote ilimalizwa baada ya kuanguka kwa taifa la Israeli, watu walipokuwa katika kifungo cha Babeli.

### **MUHTASARI WA 1 WAFALME**

1:1-4:34	Sulemani aimarisha ufalme wake
5:1-9:25	Majengo ya Sulemani
9:26-11:43	Mambo mengine katika utawala wa Sulemani
12:1-16:28	Siku za kwanza katika ufalme uliogawanyika
16:29-22:53	Huduma ya Eliya